




Mod aliquwa
amechoka kuishi
majini.




"Jihadhari. Ngozi
yako itanyauka,"
Kasa alimwonya.



Lakini, Mod alitaka
kujua.

Aliruka akaenda zake.



Alitazama kila mahali.



Alikuta kinyonga
wa kizambarau.
Alikuwa kando ya
dimbwi la maji.



Kinyonga aligeuka
rangi ya waridi!
Mod aliruka mbali
naye.



Alimwona fisi
akikoka moto.




Moto ulienea
karibu na
Mod. Aliogopa.



Moto uliichoma
ngozi yake.

Aliruka ndani ya
dimbwi la maji.



Lakini ngozi yake
ilikuwa tayari na
malengelenge.



Mod alipata ngozi
kavu na mbaya.

Alianza kuishi
miambani.



Vyura wachache
wana ngozi nyororo.

Wanaishi majini.